# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA

# MANYARA











Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan

## HOSPITALI YA RUFAA MKOA WA MANYARA YAJIVUANIA MAFANIKIO LUKUKI MIAKA MITATU YA RAIS DK SAMIA











Mganga mfawidhi Hospitali ya Rufaa mkoa wa manyara Dk. Katherine Magali

MAFANIKIO

# Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Manyara yajivuania mafanikio lukuki Miaka mitatu ya Rais Dk. Samia

**>>DK Magali ainisha namna walivyokamilisha ujenzi wa majengo na ununuzi wa vifaa tiba**

**>>Waeleza walivyoboresha utoaji wa huduma kwa wananchi**




Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara ipo katika makao makuu ya Mkoa wa Manyara mji wa Babati kando ya barabara kuu kutoka Arusha kwenda Singida. Mnamo 2006 Sekretarieti ya Mkoa ilipendekeza kwa serikali kujenga Hospitali ya Mkoa yenye uwezo wa vitanda 350 ambavyo vitatoa huduma za afya kwa ujumla na maalum.

Baada ya maandalizi yote muhimu ikiwa ni pamoja na kupata ardhi na mita za mraba 67,334 na fedha za ujenzi zilifanyika. Mnamo 2009 ujenzi halisi wa Hospitali ulianza na iliamuliwa kuwa katika awamu. Serikali ilikubali kutoa jumla ya Tshs. Bilioni 16.5 kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa vifaa vya matibabu.

Awamu ya kwanza ilihusisha ujenzi wa wadi ya wajawazito, ambayo imekamilika na sehemu ya vifaa. Sehemu ya maabara pia ilikamilishwa katika awamu hii kwa kutumia Mfuko wa Abbot. Awamu ya pili ni pamoja na ujenzi wa nyumba ya kufulia, kufulia na ujenzi wa incinerator. Majengo haya yanatumika. Awamu ya pili pia ilijumuisha tanki la maji la chini ya ardhi, nyumba ya walinzi na uzio wa Hospitali.

Hospitali ilianza kufanya kazi mwezi Aprili 2013 kwa kutoa OPD, kliniki maalum (Wagonjwa ya kisukari, shinikizo la damu, kifua kikuu na VVU), meno, Jicho, Maabara, kumbukumbu za Matibabu, sauti ya Ultra na maduka ya dawa, huduma za afya ya uzazi na watoto. Mnamo Mei 2014, Hospitali ilianza kutoa huduma za idara ya wagonjwa na Mei 2015 Hospitali ilianza kutoa huduma za uzazi, huduma za kujifungua na upasuaji. Kufikia mwaka 2016 hadi 2018 Hospitali iliendelea kupanua huduma zake kama ifuatavyo; kufunga mifumo ya elektroniki (GoT-HMIS na CRDB) kwa usimamizi wa rasilimali, kusanidi mitandao ya Hospitali (LAN) kuwezesha mawasiliano, utangulizi wa huduma maalum katika dawa za ndani, watoto, upasuaji, vizuizi na idara ya magonjwa ya akili, uanzishaji wa idara ya matengenezo, uanzishwaji wa idara ya ukarabatiji , Idara ya biomedical na ICU .

**MAFANIKIO**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa mkoa wa Manyara Dk Katherine Magali akieleza mafanikio yaliyopatika katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Dk Samia Suluhu Hassan katika hospitali alisema wamepata mafanikio mengi ambayo wanajivunia ikiwemo

majengo ya kisasa ya kutolea huduma za Afya ikiwemo huduma ya Radiolojia ambapo jengo hilo liligharimu kiasi cha shilingi mil 370, jengo la magonjwa ya dharura liligharimu mil 650 na jengo la wagonjwa mahututi (ICU) liligharimu shilingi mil 560 ambapo kwa sasa jengo linalotimika ni Radiolojia na huduma zake zinaendelea.

Pia Dk magali alisema walifanikiwa kupokea CT-Scan ambayo ina thamani ya shilingi Bil 1.8, na vifaa tiba yenye thamani ya shilingi Bil 3.4

Aidha alisema katika miaka hii mitatu ya Rais Dk .Samia madarakani wamefanikiwa kupata Jengo la Mtumishi lenye thamani ya shilingi Mil 90 ambapo jengo hilo limekamalika na linatumika.

Pia wamefanikiwa kupata Mtambo wa Kuzalisha Hewa Tiba ya Oksijeni yenye thamani ya shilingi mil. 600 na wanaidadi ya Mitungi 390.

"Kama Hospitali kweli tunajivunia baada ya kupata sisi pamoja na vituo ambavyo vipo karibu yetu wote wanapata huduma ya Oxygen kupitia mtambo huu kwa hiyo wagonjwa wa kulazwa na waliopo nje wanapata " amesema Dk Magali.

Alisema kama Hospitali kwa kipindi hiki cha miaka mitatu ya Rais Samia wamefanikiwa kufanya utanuzi wa baadhi

**Tumepata ongezeko la madaktari bingwa wa mama na mtoto ambapo kwa upande Mama na Uzazi awali tulikuwa na daktari 1 ambapo ameongezeka mmoja na kwa sasa watakuwa wawili na madaktari Bingwa wa Upasuaji wapo 2 na madaktari bingwa wa magonjwa ya dharura 2 ambao wameongezeka kwa kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan**



**Mganga mfawidhi Hospitali ya Rufaa mkoa wa manyara Dk. Katherine Magali**









MAFANIKIO

# MAFANIKIO YA MIAKA MITATU YA RAIS DK, SAMIA KATIKA SEKTA YA AFYA NCHINI,



Mashine ya CT-Scan

ya huduma ikiwemo eneo la kulaza wenye Bima, kulaza wagonjwa wa VIP, wagonjwa wa Private

Dk.magali alisema katika kipindi hiki wamefanikiwa kupata ongezeko kubwa la watumishi ambapo kwa kipindi chote walikuwa na watumishi 130-200 ambapo mpaka sasa wameongezewa watumishi 278 ambao wanafanya kazi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara wa kada mbalimbali wakiwema Madaktari Bingwa na wataalamu wengine .

"Tumepata ongezeko la madaktari bingwa wa mama na mtoto ambapo kwa upande Mama na Uzazi awali tulikuwa na daktari 1 ambapo ameongezeka mmoja na kwa sasa watakuwa wawili na madaktari Bingwa wa Upasuaji wapo 2 na madaktari bingwa wa magonjwa ya dharura 2 ambao wameongezeka kwa kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan" amesema Dk Magali.

Alisema Lakini Upatikanaji wa Dawa katika kipindi hiki cha Miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan kumekuwa na mabadiliko mengi ambayo yamevutia uwepo wa upatikanaji wa dawa ambapo kwa sasa wanaasilimia 95-98 ya upatikanaji wa dawa.

Alifafanua kwamba kuna njia mbalimbali ambazo zipo za upatikanaji wa dawa ikiwemo duka la Bima,duka wagonjwa wanaonunua dawa,duka linalojitegemea lenyewe


Alieleza kwamba kila robo mwaka wao kama Hospitali wanawezeshwa kutoa huduma za

**Tumepata ongezeko la madaktari bingwa wa mama na mtoto ambapo kwa upande Mama na Uzazi awali tulikuwa na daktari 1 ambapo ameongezeka mmoja na kwa sasa watakuwa wawili na madaktari Bingwa wa Upasuaji wapo 2 na madaktari bingwa wa magonjwa ya dharura 2 ambao wameongezeka kwa kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan**

kibingwa kwa kuzunguka katika wilaya zilizopo mkoa wa Manyara sambamba na kuwaalika madaktari bingwa kwa fani ambazo hazipo ndani ya Hospitali ili wateja wao waweze kupata huduma hapo.

Amesema katika kipindi hiki cha miaka mitatu ya Samia Suluhu Hassan idadi ya watumishi imeongezeka hadi kufikia 278, watumishi wamefanikiwa kupata stahiki zao ikiwemo kupandishwa madaraja hata wale waliotakiwa kubadilishwa kada wamefanikiwa kubadilishwa kada ambapo jumla ya watumishi 70 wameweza kubadilishwa kada na wengine kupandishwa


Mitungi ya ges


Vifaa tiba vilivyopo katika chumba cha wagonjwa wa dharura



**Mitungi ya kuzalisha gesi.**

# MAFANIKIO YA MIAKA MITATU YA RAIS DK. SAMIA KATIKA SEKTA YA AFYA NCHINI

vyeo

Pia wamefanikiwa kupata Ufadhili wa Masomo kwa watoa huduma za Afya ikiwemo Madaktari Bingwa na wataalamu wengine

Kusogeza Huduma za Kibingwa kwa Wananchi ikihusisha ufanyikaji wa kambi za Kibingwa Hospitalini pamoja na kliniki mkoba zinazofanyikakatika kila robo ya mwaka pamoja na Ongezeko la Stahiki za watumishi pamoja na upandaji wa madaraja kwa wakati

### MIKAKATI

Dk Magali alisema mikakati ya kuendelea kufanya vizuri zaidi kwa kipindi hiki cha miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kupata mtaji yaani kwa kupata majengo,watumishi,vifaa Tiba kama hospitali wamejipanga kuendelea kukusanya fedha ambazo zitawasaidia kuendeleza kuongeza vifaa tiba kwa ajili ya kuendelea kuboresha huduma,kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapeleka wengine masomoni.

"Ukiacha masomo ya mda mrefu lakini baadhi watumishi tunawapeleka mafunzo ya mda mfupi kwa ajili ya kupata ujuzi mbalimbali na hapa hapa Hospitali pia tunatoa mafunzo kwa watumishi juu ya utoaji wa huduma bora na mafunzo ya hivi vifaa tiba tulivyonavyo ili waweza kuvitumia vyema maana unaweza ukawa na vifaa tiba lakini usiweze kuvitumia" alisema Dk.Magali

### MIPANGO YA BAADAE

Kwa mujibu wa Dk Magali alisema wanampango wa kumalizia majengo ambayo yapo na hayajakamilika vizuri kupitia mapato ya ndani ili waendelee kuboresha huduma lakini pia wanampango wa kufanya ukarabati wa majengo ya zamani ambayo wamejipanga kuendelea kuyaboresha kupitia fedha ambazo wanazipata.

"Tunajengo la mochwari, tuna jengo la Laundry, jengo la mama na mtoto,maabara, kwa hiyo haya majengo yote sisi tunaendelea kuyaboresha" alisema.

**Ukiacha masomo ya mda mrefu lakini baadhi watumishi tunawapeleka mafunzo ya mda mfupi kwa ajili ya kupata ujuzi mbalimbali na hapa hapa Hospitali pia tunatoa mafunzo kwa watumishi juu ya utoaji wa huduma bora na mafunzo ya hivi vifaa tiba tulivyonavyo ili waweza kuvitumia vyema maana unaweza ukawa na vifaa tiba lakini usiweze kuvitumia**

Aidha alisema wanampango wa kuongeza huduma mpya ambazo wananchi wa mkoa wa Manyara na walioko jirani watafanikiwa kupata huduma hizo kwa ukaribu zaidi.

Alizitaja huduma hizo mpya ni pamoja na kusafisha figi (Dialysis) ambayo itaanza mwaka ujao wa fedha,huduma ya fast track kwa wateja wanaokuja Hospitali,wanampango wa kuanzisha sehemu za kutengeneza maji ya drip,kuhakikisha dawa zinapatikana kwa wakati.

### MIRADI

Akifafanua zaidi miradi inayoendelea kwa kipindi hiki cha miaka mitatu ya Rais Samia Suluhu wamepatiwa majengo lakini kuna baadhi hayajamaliiziwa ikiwemo jengo la magonjwa ya dharura ambalo bado halijamalizika lakini kama Hospitali wamejipanga kumalizia kwa kipindi hiki cha mwaka wa fedha ambapo zitatumika fedha za ndani ikiwemo kumalizia umeme na kumalizia kuingiza gesi Tiba.

### SHUKRANI

Alisema wanapenda kumshukuru Mh.Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha za kuwezesha ujenzi,maboresho ya huduma ambazo zinaendelea kwa kuendelea kuwaletea wataalamu wa fani mbalimbali wanaendelea kuwapata,kuwaletea vifaa tiba ambavyo kwa sasa wanajivunia kwa kuwa huduma zimekuwa bora sana baada ya kuongezewa vifaa hivyo.

Pia alishukuru kwa ujenzi unaendelea ambapo hayo yote yatafanya sehemu zao wanazotolea huduma ambazo zilikuwa zinamsongamano basi zitapunguza msongamano maeneo hayo.

### WITO

Aidha Dk Magali ametoa wito kwa jamii waendelea kuiamini Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara waendelee kujivunia uwepo wa Hospitali hiyo kwa kuwa wamejipanga kutoa huduma za rufaa katika ngazi zote za utoaji huduma ikihusisha wataalamu,madaktari bingwa na watia huduma wengine ,

vifaa tiba vya kisasa, vipimo vya kimaabara na dawa.




**Jengo la idara ya Radiolojia**






**Wahandisi wa vifaa tiba wakijaza gesi kwenye mitungi**



**Mhandisi Salaila Nyangoi vakijaza gesi kwenye mitungi ya ges**